# USAWIRI WA ESKATOLOJIA YA WAAFRIKA KATIKA MBOLEZI ZA WANGONI

*Martina Duwe*
*Chuo Kikuu Mzumbe – Tanzania*
*magriccola@gmail.com*

## Ikisiri

*Eskatolojia ni kipengele kimojawapo kinachodhihirisha falsafa ya jamii za Waafrika kulingana na mila na desturi zao. Tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu dhana hii zimejiegemeza katika muktadha wa kiteolojia. Baadhi ya tafiti hizo ni zile zilizofanywa na Baloyi (2008) na Lup (2013). Licha ya kuwapo kwa tafiti hizo, dhana ya eskatolojia ya Waafrika hususani fasihi simulizi za jamii ya Wangoni bado haijamakinikiwa ipasavyo. Aidha, ni wazi kwamba fasihi simulizi ni fasihi inayobeba na kuibua maarifa ya kifalsafa yanayoisawiri jamii husika kulingana na kaida zao. Kwa mantiki hiyo, makala hii inajadili usawiri wa eskatolojia ya Waafrika katika kipera cha mbolezi hususani za jamii ya Wangoni ili kubainisha maarifa yanayobebwa katika kipera hicho. Makala hii ni matokeo ya utafiti uliofanyika kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji shirikishi katika matukio yanayoambatana na suala la kifo na mahojiano ya ana kwa ana na baadhi ya Wangoni katika mazingira yao halisi. Data zimechanganuliwa kwa njia ya maelezo. Data hizo zinaonesha kuwapo kwa eskatolojia ya Waafrika katika mbolezi za jamii hiyo. Hata hivyo, makala hii inajadili vipengele muhimu vitatu tu ambavyo ni: kuamini katika uwepo wa Mungu, mwendelezo wa maisha baada ya kifo na nguvu za waliokufa (mizimu).*

## 1.0 Utangulizi

Eskatolojia ni tawi mojawapo la teolojia. Dhana hii imefasiliwa katika mitazamo tofautitofauti. Kwa jumla, mitazamo hiyo tunaweza kuimulika kwa namna kuu mbili. Mtazamo wa kwanza, unaifasili dhana hii kwa kuihusisha na imani ya dini anayoamini mtu katika mazingira yake halisi. Wadau wa mtazamo huu wanasema kuwa eskatolojia ni tawi mojawapo la teolojia linalojihusisha na ufafanuzi wa fikra za mwanadamu katika kuufikia mwisho na maisha yake baada ya kifo kwa kuhusisha misingi ya utamaduni wa imani ya dini katika ulimwengu wake (Oxford, 1989; Lup, 2013). Mtazamo wa pili, unaifasili dhana hii kwa kujiegemeza katika imani ya dini ya Kikristo pekee.

Wataalamu wanaoshadidia mtazamo huu wanaona kuwa eskatolojia ni tawi mojawapo la dini ya Kikristo linalojihusisha na suala la kifo kwa aaminiye na maisha yake baada ya kuja kwa Kristo (Masihi) mara ya pili (Bujo, 1998; Shields, 2008). Katika makala hii, tumeishughulikia dhana hii kwa kujiegemeza katika mtazamo wa kwanza unaoitazama dhana hii kama taaluma inayohusika na uchunguzi wa fikra za mwanadamu kuhusu hatima yake ya maisha na maisha baada ya kifo kulingana na misingi ya imani anayojiegemeza nayo.

Eskatolojia ni msamiati unaotokana na neno la Kiingereza "*eschatology*". Neno hili limeundwa kwa maneno mawili ambayo ni "*eschatos*" (*last*) maana yake ni mwisho na "*logy*" (*the study of*) ni uchunguzi wa jambo fulani. Asili ya dhana hii ni huko Ugiriki ambako ilianza kutumiwa na wanafalsafa katika miaka ya elfu moja mia saba na kushika kasi katika miaka ya elfu moja mia nane (Lup, 2013). Taaluma hii ilitumika kwa lengo la kutafiti kuhusu hatima ya vitu, hususani mwanadamu katika ulimwengu wake. Kimsingi, taaluma hii iliibuka kutokana na mijadala ya wanafalsafa juu ya kutafuta ukweli wa maswali kama vile: Je, umri halisi wa ukomo wa maisha ya mwanadamu ni upi? Je, mwanadamu anafikiri nini kuhusu hatima yake, hukumu na maisha baada ya kifo? Je, Mungu ana nafasi gani katika uhai wa mwanadamu (Shields, 2008; Lup, 2013). Kila jamii ina miongozo na taratibu zinazotumika katika kuliendea suala la hatima yao.

Fikra za Waafrika juu ya hatima na mwendelezo wa maisha yao baada ya kifo kwa kujiegemeza katika imani walizonazo, ndiyo eskatolojia yao. Fikra hizo zinabainika kupitia tamaduni zao za namna ya kuliendea suala hilo ambapo huamini katika masuala mbalimbali. Baadhi ya masuala yanayoaminiwa na Waafrika ni: dhana kuhusu maisha baada ya kifo na mizimu ina nguvu katika maisha ya walio hai.

Ndiyo sababu, katika kuishi kwao wanaomba jambo walitakalo kupitia mizimu hiyo. Pia, waliokufa bado roho zao zinaendelea kuishi katika ulimwengu wa waliohai (Ramose, 2002; Baloyi, 2008). Masuala mengine yanayoaminiwa na Waafrika kuhusu hatima yao ni: kifo ni jambo la lazima kwa kila mwanadamu na Mungu yupo katika safari ya kuifikia hatima yao (Mbiti, 1990; Bujo, 1998). Aidha, Waafrika wanaamini kuwa, mtu akifa huwasiliana na waliohai kupitia ndoto. Sambamba na hayo, kifo cha mwanadamu huhusishwa na sababu fulani za kutokea kwake (Baloyi, 2008). Kwa msingi huo, hakuna kifo cha mwanadamu kisichokuwa na sababu kulingana na tamaduni za Waafrika. Fikra hizi hubainika katika matukio mbalimbali yanayoambatana na suala la kifo. Hivyo basi, katika makala hii tunajadili baadhi ya masuala hayo ambayo ni: kuamini katika uwepo wa Mungu; mwendelezo wa maisha baada ya kifo na nguvu za waliokufa (mizimu) kwa kujiegemeza katika mbolezi za Wangoni.

Waafrika hutumia vijenzi mbalimbali wakati wa kuomboleza ikiwamo mbolezi zinazokidhi tamaduni za kuamini katika miungu yao (Samuel, 1955). Mbolezi ni nyimbo za maombolezo ambazo huimbwa pale panapotokea kifo cha mwanadamu (Mulokozi, 2017). Hivyo, mbolezi hutumiwa na jamii nyingi za Waafrika katika matukio mbalimbali yanayohusiana na suala la kifo kama vile: ibada za mazishi pamoja na shughuli za matanga. Mbolezi zinapoimbwa huwasilisha maudhui yanayoisawiri jamii husika. Aidha, hubeba fikra zinazoonesha hisia na mwelekeo wao wa kulitazama na kuliendea suala la hatima/miisho yao.

Wangoni ni miongoni mwa jamii za Kiafrika ambao hupatikana katika maeneo mbalimbali barani humo. Nchini Tanzania, tunapoyataja makabila mbalimbali yanayoishi katika nchi hiyo, ni wazi kuwa Wangoni ni kabila linalojibainisha kwa sifa mahususi za kijamii, kiuchumi na kitamaduni (Mapunda, 2016). Kabila hili hupatikana Kusini mwa nchi ya Tanzania katika mkoa wa Ruvuma. Pamoja na hilo, katika ujio wao, waliweza kuishi katika maeneo mbalimbali nchini Tanzania. Maeneo hayo ni kama vile: katika ardhi ya Unyamwezi, Ufipa na Usukuma (Ebener, 2009). Katika maeneo hayo, walijulikana kwa jina la Watuta. Makundi yaliyokwenda huko yalikuta makundi ya wenyeji yakiwa na nguvu kubwa ya kiutawala na hivyo, kuishi kwa kufuata tamaduni walizozikuta katika maeneo hayo. Mkoani Ruvuma, hili ndilo kabila kuu ambapo ndani yake tunazungumzia makabila mengine mengi yakiwamo ya Wamatengo, Wandendeule na Wayao (Ngonyani, 1989). Katika kubainisha tamaduni zao, kuna vipengele vinavyowaunganisha na kujulikana kama kabila moja lenye kaida zinazofanana.

Hata hivyo, utafiti ulijiegemeza katika tarafa ya Maposeni iliyopo katika halmashauri ya Songea pekee.

## 2.0 Kiunzi cha Nadharia

Mjadala wa makala hii unaongozwa na Nadharia ya Ujaala. Hii ni nadharia mojawapo inayotumika katika kuhakiki kazi mbalimbali za kifasihi. Mtazamo mkuu wa Wanaujaala ni kuamini kwamba maisha ya mwanadamu pamoja na matendo yote ayatendayo katika ulimwengu wake, vinatawaliwa na kuongozwa na nguvu za Mungu (Jaala) wake (Wamitila, 2002). Hali hii ni kutokana na ukweli unaoaminiwa kuwa pasipo nguvu za Jaala mwanadamu hawezi kufanya jambo lolote katika maisha yake. Naye, Ponera (2014) anashadidia hoja hii kwa kusema kuwa Ujaala ni nadharia inayojinasibisha na dini ya mwanadamu ambapo anaamini vitu vyote na mambo yote yaliyoko na ayatendayo katika dunia yake ni kwa uwezo wa Jaala (Mungu). Kazi zote za kisanii pamoja na mambo yamtokeayo mwanadamu hutokana na nguvu zake. Mtazamo huu unajipenyeza katika fikra za mwanadamu ambapo anayatazama maisha kuanzia mwanzo hadi hatima (mwisho) yake kwa kujiengemeza katika imani ya nguvu na uwezo wa Mungu wake.

Chimbuko la nadharia hii ni fikra za wanafalsafa wa awali kutoka Ugiriki ya Kale hususani Aristotle na Plato ambapo kazi zao za kisanaa zilionekana kuakisi dhana ya Ujaala (Ponera 2014). Baadaye, wanafalsafa kutoka pande mbalimbali za ulimwengu, waliendelea kuchunguza maisha ya jamii na kuonesha yaliyomo kwa kujiegemeza katika misingi ya nadharia hii. Kwa upande wa Afrika, Murphy (2003) anasema kwamba kihistoria, Ujaala wao ulizingatia masuala makuu mawili ambayo ni miungu na mizimu. Kwa mujibu wake, Waafrika huamini katika nguvu na uwezo wa Mungu kupitia miungu na mizimu kulingana na tamaduni za jamii husika. Masuala hayo katika maisha yao, hutazamwa kama daraja muhimu la kupeleka maombi na sala kwa Mungu wao wa kweli. Kwa hiyo, nadharia hii imetumika kama mwegamo mkuu katika kuchunguza na kujadili kuhusu usawiri wa eskatolojia ya Waafrika katika mbolezi za Wangoni.

## 3.0 Methodolojia ya Utafiti

Makala hii imetokana na uchunguzi uliofanyika katika mwegamo wa kitaamuli. Huu ni mwegamo unaomhitaji mtafiti kutumia tafakuri ya kina katika kupembua na kuhusianisha taarifa mbalimbali zilizopatikana uwandani na kutoa ufafanuzi kwa kuzingatia misingi ya nadharia husika pamoja na ithibati bayana (Ponera, 2019). Kwa hiyo, data zimewasilishwa kwa njia ya maelezo. Haya ni matokeo ya uchunguzi ulifanyika katika vijiji vya Lugagara, Maposeni, Mgazini na Mdunduwalo vilivyopo katika Halmashauri ya Songea Vijijini, mkoani Ruvuma. Uteuzi wa maeneo haya ulizingatia kigezo kwamba, jamii hiyo bado inaishi kwa kufuata tamaduni zao, tofauti na wale waishio katika maeneo ya mijini. Hivyo, mbolezi zinazotumika zaidi kama kijenzi muhimu cha kuomboleza katika matukio mbalimbali yanayoambatana na suala la kifo (Mapunda, 2016). Hii imesaidia katika kuthibitisha eskatolojia ya Waafrika inavyosawiriwa katika mbolezi hizo kama kipera kimojawapo cha fasihi simulizi. Aidha, mbinu ya ushuhudiaji shirikishi katika matukio yanayoambatana na suala la kifo hususani wakati wa ibada za mazishi na matanga ilitumika. Ushuhudiaji huo ulifanyika pia katika shughuli zinazoambatana na ufanywaji wa matambiko katika vijiji lengwa. Pia, mahojiano ya ana kwa ana na baadhi ya Wangoni hususani wazee na waimbaji katika matukio yanayombatana na suala la kifo, yalifanyika kwa madhumuni ya kupata data mbalimbali za utafiti huu.

## 4.0 Eskatolojia ya Waafrika katika Mbolezi za Wangoni

Ifahamike kuwa mbolezi za Wangoni za sasa, zimepitia mabadiliko mengi yaliyosababishwa na mwingiliano ya kijamii hususani dini ya Kikristo na athari za matumizi ya lugha ya Kiswahili. Hali hii imesababisha mbolezi za asili za lugha ya Kingoni kuingizwa msamiati wa lugha ya Kiswahili. Kwa mantiki hiyo, imebainika kwamba mbolezi nyingi zina mseto wa lugha (Kingoni na Kiswahili) na baadhi zipo katika lugha ya Kiswahili pekee. Hii ni kutokana na athari ya uimarikaji wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika maeneo hayo. Hata hivyo, uimbaji na uwasilishaji wa maudhui husawiri misingi ya maisha ya jamii hiyo. Hii ni kutokana na uchopekaji wa vionjo mbalimbali vinavyoakisi utamaduni wao katika viitikio au vibwagizo. Sambamba na hilo, imebainika kuwa hakuna ulinganifu wa uingizwaji/uchopekaji wa vionjo hivyo wakati wa uimbaji wa mbolezi zao. Vionjo hupachikwa kutegemeana na mazingira ya msiba husika na umahiri wa mwanzishaji na/au waitikiaji kwa jumla. Jambo hili huleta utofauti fulani wa namna ya msikiko na msamiati unaoingizwa katika mbolezi ya aina moja. Licha ya kuwapo kwa mabadiliko ya namna ya kuiendea eskatolojia yao kupitia mbolezi hizo, imebainika kuwa, bado fikra za jamii hiyo juu ya hatima yao hazijaathiriwa na jambo lolote.

Katika makala hii tumezimulika mbolezi zote (zenye mseto wa lugha na za Kiswahili). Aidha, ufafanuzi uliotolewa kwa lugha ya Kingoni umetafsiriwa ili kuakisi asili ya lugha ya makala hii. Hali hii ni kutokana na kuamini kwamba suala la lugha inayotumika kama chombo cha mawasiliano, haliwezi kuondoa fikra/mitazamo ya mwanadamu katika kulimulika na kuliishi jambo fulani.

**4.1 Kuamini katika Uwepo na Nguvu za Mungu**

Suala la kuamini katika nguvu za Mungu ndio msingi wa imani ya dini yoyote anayofungamana nayo mwanadaamu. Wangoni kama walivyo Waafrika wengine, huamini suala la uwepo na nguvu za Mungu katika maisha yao. Huamini kuwa, yeye ndiye huamuru na kuruhusu kutokea kwa mwanadamu (kuzaliwa) katika ardhi aliyoipanga yeye. Kwa kujiegemeza katika Nadharia ya Ujaala, jamii hiyo huamini kwamba uhai na uzima wa kila mwanadamu hutegemea nguvu za Mungu kwa kuwa ndiye asili ya vyote vilivyopo ulimwenguni. Vivyo hivyo, hatima ya maisha ya mwanadamu hupangwa naye pasipo mwanadamu huyo kufahamu wakati na mahali itakapotokea hatima hiyo. Huamini kuwa kifo ni safari ya kuelekea kwa Mungu. Hivyo, wanapoimba katika matukio mbalimbali yanayoambatana na suala la kifo, mbolezi zao hudhihirisha fikra hizi. Jambo hili linabainika wazi kupitia wimbo unaoitwa "*Aga Mang'ova*"[1]**.** Unaimbwa hivi:

**Kiitikio**: *Gena (aga) mang'ova, mang'ova nitamayi na yani*
*pa nyumba* [2]*(huyu baba) ahambili* [3] kwa Mungu ehee
(x2)

Sasa siku imekwisha *aga mang'ova, mang'ovaga*,
Kwake Mungu apandisha *aga mang'ova, mang'ova*.

Moyo wake wa shukrani *aga mang'ova, mang'ovaga*,
Apumzike kwa amani *aga mang'ova, mang'ovaga.*

Mema mengi umempa *aga mang'ova, mang'ovaga*,
Ameshindwa kukulipa *aga mang'ova, mang'ovaga*.

Baba mwema ondolea *aga mang'ova, mang'ovaga*,

---

[1]. *Gena (aga) mang'ova* maana yake katika lugha ya Kiswahili ni hizi/haya makazi yaliyoachwa baada ya watu/mtu kuhama au kufa.
[2]. *Nitamayi na yani pa nyumba* ni sentensi inayomaanisha nikae na nani hapa nyumbani.
[3]. *Ahambili* ni msamiati unaomaanisha 'amekwenda'.

Yote aliyokukosea *aga mang'ova, mang'ovaga*.

Yesu mpenzi umjie *aga mang'ova, mang'ovaga*,
Ombi letu usikie *aga mang'ova, mang'ovaga*.

Umfiche mtoto wako *aga mang'ova, mang'ovaga*,
Ndani ya jeraha zako *aga mang'ova, mang'ovaga*.

Twaiweka roho yake *aga mang'ova, mang'ovaga*,
Mikononi mwako baba *aga mang'ova, mang'ovaga*.

Bila hofu apumzike *aga mang'ova, mang'ovaga*,
Mwisho kwake afike *aga mang'ova, mang'ovaga***.**

**Chanzo**: Utafiti (2019)

Mbolezi hiyo inaonesha kuwa anayekufa anakwenda kwa Mungu. Hizi ni fikra za kijaala ambapo Mungu hutazamwa kama nguzo muhimu katika suala la asili na hatima ya mwanadamu. Hii ni kwa sababu yeye ndiye anayetoa uhai na kumwongoza mwanadamu katika kila jambo. Aidha, hatima ya mwanadamu huyo, nayo huidhinishwa naye pasipo majadiliano na yeyote. Fikra hizi husawiri eskatolojia ya Waafrika inayojiegemeza katika kumtazama Mungu kama sababu ya kutokea kwa jambo lolote katika maisha ya mwanadamu likiwamo suala la kifo.

Sambamba na hilo, mhojiwa mmoja anathibitisha jinsi jamii hiyo inavyoamini katika uwepo wa Mungu maishani mwao. Anasema:

> *Tete timanyili naha kila munu ahumili kwa Chapanga. Ndi mana ati pa tiyimba nyimbu za malilu tilasa kwa ahumili munu na kwa ihamba. Tikita naha ili kulasa mambo ga iweza kwa munu waki mwa amuhumbili na kumvika pa dunia apa. Tavangoni tawanzili kadeni kummanya Chapanga hata kabula ya kubwela vamisheni ava. Va gogo vitu vavililepa na likanisa lakini vammanyili Chapanga na vene. Te tukumueshimu kweli Chapanga. Takavyai kumavembo tukumvembela mwene ndi Chapanga wa kila cha tikita. Tukumuwomba mwene ampokelayi mlongo witu kwa ihamba. Te malilu tigalokesa chiimani kufwatana na chatitama. Tisali na kuyimba nyimbu za malilu ili kumwombela kwa Chapanga.*

Sisi tunajua kwamba kila mwanadamu ametoka kwa Mungu. Ndiyo sababu tunavyoomboleza tunaimba nyimbo mbalimbali zinazoonesha mwanzo wa mwanadamu na mwisho wake ni Mungu mwenyewe. Hii yote ni kufafanua ukuu na uwezo wake kwa mwanadamu aliyemuumba na kumweka duniani. Wangoni hata kabla ya ujio wa Wamisionari, tulikuwa tunaamini katika uwapo na nguvu zake Mungu. Mababu zetu hawakuwa na kanisa kama ilivyo sasa, lakini walimjua Mungu. Sisi tuna mheshimu sana Mungu. Tunapokuwa katika hali ya huzuni, tunamlilia kwa kuwa tunaamini kuwa yeye ndiye mpangaji wa mambo yote. Daima tunaomba kwake ili ampokee ndugu yetu katika makao mapya. Kifo kwetu kinatazamwa kiimani zaidi kulingana na tunavyoishi. Hivyo, tunasali na kuimba nyimbo mbalimbali za huzuni zenye kuelekeza maombi yetu kwa Mungu (Tafsiri yangu).
**Chanzo:** Utafiti (2019)

Maelezo hayo yanatuthibitishia bayana kuwa suala la kuamini katika nguvu na uweza wa Mungu ni suala linalofikiriwa na wanajamii. Hivyo, Wangoni huamini kuwa yupo Mungu katika nyakati zote za maisha yao. Ndiyo sababu hata wakati wa hatima yao humkimbilia yeye kwani huamini kuwa kila jambo linalotokea huwa linakuwa limepangwa naye. Hii ni eskatolojia ya Waafrika ambapo huamini katika nguvu na uwezo wa Mungu kama suala linalosababisha hatima yao. Mungu kama hajaamua mwanadamu afe, basi hata apate tabu ya namna gani ikiwamo ugonjwa wa muda mrefu hawezi kufa mpaka siku zilizopangwa naye zitimie. Hivyo basi, eskatolojia ya Waafrika husawiriwa vema katika fasihi simulizi ya jamii ya Wangoni hususani mbolezi.

**4.2 Mwendelezo wa Maisha Baada ya Kifo**

Wangoni kama jamii mojawapo ya Waafrika, wanaamini kuwa kuna mwendelezo wa maisha baada ya kifo. Hivyo, mwanadamu akishakufa anaendelea tena kuishi katika ulimwengu mwingine. Ulimwengu huo ni makao mazuri ambayo yameandaliwa na Mungu mwenyewe. Katika suala hili, wanaamini kwamba kifo kwa mwanadamu huhusisha mwili pekee ila roho yake hurudi kule alikotoka (kwa Mungu) na huendelea kuishi tena pamoja naye kama inavyofafanuliwa na Mbiti (1990). Fikra hizi husawiriwa vema katika mbolezi zao zinazoimbwa wakati wa matanga na ibada mbalimbali zikiwamo za kuaga mwili wa marehemu na mazishi. Jambo hili linathibitishwa wazi kupitia wimbo wa Kiswahili wenye asili na mahadhi ya Kingoni unaosema “Amerudi kwake Mungu”. Unaimbwa:
**Kiitikio:** Amerudi ndugu huyo amerudi (mwana huyo)
Amerudi alikotoka amerudi (amerudi) x2

*Sasa siku imekwisha amerudi (kwake Mungu)*
*Kwake Mungu apandisha amerudi (amerudi).*

*Moyo wake wa shukrani amerudi (apumzike)*
*Apumzike kwa amani amerudi (amerudi).*

*Mema mengi umempa amerudi (ameshindwa)*
*Ameshindwa kukulipa amerudi (amerudi).*

*Baba mwema ondolea amerudi (yote aliyo-)*
*Yote aliyokukosea amerudi (amerudi).*

*Yesu mpenzi umjie amerudi (ombi letu)*
*Ombi letu usikie amerudi (amerudi).*

*Umfiche mtoto wako amerudi (ndani ya)*
*Ndani ya jeraha zako (amerudi).*

*Twaiweka roho yake amerudi (mikononi)*
*Mikononi mwako baba amerudi (amerudi).*

*Bila hofu apumzike amerudi (mwisho)*
*Mwisho kwake afike amerudi (amerudi*).

**Chanzo:** Utafiti (2019)

Katika wimbo huo tunabaini kwamba Wangoni wanaamini kuwa kifo kwa mwanadamu ni safari ya kuelekea katika ulimwengu mwingine ambapo ataendelea kuishi tena. Ndivyo ilivyo katika maisha ya Waafrika kwa jumla ambapo huamini kuwa anayekufa ataendelea kuishi tena kwa Mungu wake aliyemuumba. Mungu ameandaa makazi kwa ajili ya watu wake ili waweze kuishi huko kwa amani. Hii ni eskatolojia ya Waafrika inayojibainisha kupitia matendo yao mbalimbali. Aidha, mjadala unaonesha kwamba kinachoendelea kuishi baada ya kifo cha mwanadanmu ni roho yake kwa kuwa ndiyo iliyowekwa na Mungu katika ukamilisho wa mchakato wa uumbaji wa mwanadamu. Katika hili, mhojiwa mmoja anaeleza:

> Mwili wa mwanadamu ni takataka kama taka tunazoziona jalalani. Kwa sababu, baada ya kifo mwili hauna thamani tena mbele za waliohai na mbele ya Mungu aliyemuumba mwanadamu

> huyo. Sisi tangu zamani tunaamini kwamba, roho ya mwanadamu haifi, kinachokufa ni mwili pekee. Waliokufa bado wapo pamoja nasi kupitia roho zao. Imani hii inatufanya tunawasiliana nao kwa njia ya kiroho. Masuala kama vile *mahoka*[4] ni uthibitisho tosha kwamba, roho zao zinaendelea kuishi kwa Mungu na katikati yetu. Tunaomba kutimiziwa mahitaji yetu kupitia wao na tunafanikiwa. Hata kama tunakwenda kanisani, bado hatuachi kuomba *mahoka* yatusaidie katika masuala mbalimbali yanayotusibu. Hii ni kutokana na kuamini kwamba, roho zao zipo pamoja nasi. Imani hii haijaanza leo, tangu zamani wazee wetu walikuwa wanatufundisha kuhusu kuheshimu na kutii waliokufa kwa kuwa bado roho zao zipo hai katika maisha yetu.
>
> **Chanzo:** Utafiti (2019)

Maelezo hayo yanatuthibitishia kwamba mwili wa mwanadamu hauna mwendelezo wa kuishi baada ya kifo chake. Ndiyo sababu umelinganishwa na takataka zinazotupwa jalalani na mwanadamu. Roho pekee ndiyo yenye uwezo huo kwa kuwa ni kiungo kilichofanyizwa na Mungu kuwa hai daima. Hizi ni fikra za Kijaala ambapo jamii hiyo humtazama Mungu wao kama mhifadhi wa roho za waliokufa.

### 4.3 Nguvu za Waliokufa (Mizimu)

Wangoni kama zilivyo jamii nyingine zilizopo Afrika huamini kwamba ndugu zao waliokufa wana nguvu kubwa sana katika kufanya maisha yao yaweze kustawi au la. Hali hii huwafanya waamini na kutenda shughuli mbalimbali kwa lengo la kuwafurahisha na kuwaridhisha ndugu zao waliokufa. Masuala hayo hufungamanishwa na ufanywaji wa matambiko yanayoambatana na sadaka maalumu kwa ajili ya *mahoka* (mizimu). Huamini kwamba mizimu ni roho ya mtu aliyekufa inayodhaniwa kuwa hai na yenye nguvu ya kutenda mambo mbalimbali kwa ajili ya waliohai. Mizimu kwao ni daraja la kufikisha maombi yao kwa Mungu wao. Fikra hizi hudhihirisha eskatolojia ya Waafrika inayojiegemeza katika suala la kuamini na kuheshimu mizimu kwa kuwa ina nguvu ya kutenda katika maisha ya waliohai. Aidha, Wangoni wanamtazama aliyekufa kwa kuhusianisha na tendo la kulala kwa roho yake. Hii ni kutokana na

---

[4]. Ni msamiati ktika lugha ya Kingoni wenye maana ya mizimu

kuamini kwamba kulala ni kupumzika tu, na hivyo, aliyelala ataamka na kuendelea kufanya shughuli mbalimbali katika mazingira yake halisi. Ndivyo inavyoaminiwa kuwa aliyekufa, ataamka au ataamshwa na waliohai ili kuendelea kutenda shughuli mbalimbali katika ulimwengu halisi. Hali hiyo hutokana na imani yao kwamba, roho ya aliyekufa ipo hai kivitendo katika maisha yao. Uhai huo wa kivitendo ndio huthibitisha kuamka kwake. Jambo hili linathibitisha eskatolojia ya Waafrika inayojiegemeza katika kuamini kuwa roho ya aliyekufa ipo hai na ina athari kubwa katika maisha ya waliohai hususani wenye uhusiano naye. Katika uombolezi wao, suala hili hubainika kupitia mbolezi mbalimbali. Mfano wa mbolezi hizo ni "Baba *Agona Mjeneza*"

**Kiitikio:** (Baabaa) Baba *angona mjeneza,*
*tee kulila* yoyoo! yoyoyooo, *tee kuliaa*! (x2)

Siku zake zimekwisha baba, baba *angona mjeneza, tee kulila*.
Kwako Mungu apandisha baba, baba *angona mjeneza, tee kulila.*

Mema mengi umempa baba ee, baba *angona mjeneza, tee kulila*.
Ameshinda kukulipa baba ee, baba *angona mjeneza*, *tee kulila*.

Baba mwema ondolea baba ee, baba *angona mjeneza, tee kulila*.
Yote aliyo kukosea baba ee, baba *angona mjeneza, tee kulila*.

Yesu mpenzi umjie baba ee, baba *angona mjeneza, tee kulila*.
Ombi lake usikie baba ee, baba *angona mjeneza, tee kulila.*

Umfiche mtoto wako baba ee, baba angona *mjeneza, tee kulila*.
Ndani ya jeraha zako baba ee, baba angona *mjeneza, tee kulila*.

Nawe mama mpe neema baba ee, baba *angona mjeneza, tee kulila*.
Raha na usiku mwema ee, baba *angona mjeneza, tee kulila.*

Roho nawe ukakeshe baba ee, baba *angona mjeneza, tee kulila*.
Pepo asimkosehe baba ee, baba *angona mjeneza, tee kulila.*

Twaiweka roho yake baba ee, baba *angona mjeneza, tee kulila.*

Mikononi mwako baba baba ee, baba *angona mjeneza, tee kulila.*

Bila hofu apumzika baba ee, baba *angona mjeneza, tee kulila*.
Mwisho kwako amefike ee, baba *angona mjeneza, tee kulila.*

**Chanzo:** Utafiti (2019)

*Angona mjeneza, tee kulila* maana yake katika lugha ya Kiswahili ni 'amelala kwenye jeneza, sisi tunalia'. Kiuhalisia, aliyelala hawezi kutenda jambo lolote litakalojidhihirisha dhahiri kwa muda huo. Lakini, anaweza kuamka kwa wakati mwingine au kuamshwa na asiyelala. Maarifa ya msingi katika mbolezi hiyo, ni kuwapo kwa uwezekano wa aliyekufa kuamka (kufanya vitendo mbalimbali katika maisha ya waliohai) kwa kuwa yupo hai. Aidha, anaweza kuamshwa na waliohai kwa mantiki kwamba kumshirikisha masuala mbalimbali yanayohusu maisha yao kwa kuwa roho yake ipo hai. Mfano wa masuala hayo ni changamoto mbalimbali kama vile magonjwa, kutokuwa na amani katika familia na kuwa na mikosi. Kwa sababu wanaamini kwamba, kufa kwake ni kama kupumzika tu lakini ana uwezo wa kutekeleza yote wanayoyahitaji kwa kuzingatia tamaduni zao. Jambo hili linadhihirisha eskatolojia ya Waafrika katika kuitazama roho kama kiungo kinachoishi na kutenda katika ulimwengu wa waliohai.

Katika kuheshimu na kutii nguvu za waliolala (mizimu), Wangoni hufanya masuala mbalimbali kwa ajili yao ikiwamo kufanya matambiko kulingana na misingi ya tamaduni zao. Wanaamini kwamba, matambiko yanasaidia kuondoa mikosi na laana zinazomwandama mtu katika maeneo mbalimbali. Baadhi ya maeneo hayo ni: mahali pa kazi, katika familia, na biashara yake. Pia, Wangoni wanaamini kuwa matambiko yana nguvu ya kuponya magonjwa yanayodhaniwa kuwa yamesababishwa na kuchukia kwa ndugu na mababu zao waliofariki (mizimu). Aidha, jamii hiyo hufanya matambiko kwa lengo la kutoa shukrani kwa mizimu baada ya kufanikiwa kwa jambo fulani katika familia au ukoo husika. Hii ni kwa sababu wanaamini kwamba kama uliomba kufanikiwa kupitia mizimu hiyo, ni vema kurudi ili kutoa shukrani baada ya kupata mafanikio yaliyoombwa. Wakati wa tambiko, mzee wa ukoo mwenye umri mkubwa ndiye anakuwa msemaji na mtoa maombi hayo nyumbani na makaburini. Mfano mzuri wa maombi yaliyoshuhudiwa katika tambiko la Wangoni ni:

***Maombi:*** *Hodi mbuya, gogo na mwavoha ya mgoni apa nayi*
*Tete tavana vinu tebwelili*

*Mtipokelei tivili apa*
*Gogo Lucasi na mbuya Namonji te tivajambusa*
*Mkotokai kuyoma pangi apo titamili magono ga mehele bila kubwela*
*kuvajambusa*
*Chondi nigalauka pai apa mkotokai kuyoma.*
*Vana vinu lelu vabwelili apa kuvajambusa*
*Mvalolali inu vanashida zavi*
*Vangi vilwala, vangi kumahengu kwavi kwambwina lepi*
*Chondi mvasaidilai vaponayi na kumahengu uko kuvyai bwina*
*Vana vavi vakasangarukai na vene vakatamai bwina*
*Vakotokai kukolewa na lipumba pa vitama*
*Mahengu gavi goha gahambai mbwina*
*Vandu voha vakavaganai na kuvatangatila pa vikwama*
*Chondi mvalingulilayi vana na vajukulu vinu ava*
*Gogo, mbuya na mwavalongo mwavoha mwa mugonili apa nayi*
*Mtipilikai kuwomba kwitu*

Hodi akina babu na bibi na wote mliolala mahali hapa
Sisi watoto wenu tumekuja
Mtupokee tupo mahali hapa
Tanawasalimu babu Lucasi na bibi Namonji
Msikasirike kwa sababu siku nyingi zimepita hatukuja kuwasalimia
Ninagaagaa hapa chini, tafadhali msikasilike
Watoto wenu wamekuja hapa leo kuwasalimia
Muwatazame na kuwasikiliza wana shida zao mbalimbali
Wengine wanaumwa na wengine hawako salama katika maeneo yao ya kazi
Chonde muwasaidie wapone na huko kazini kuwe safi
Watoto wao wakawe wazima na wao wakaishi vizuri
Wasipatwe kamwe na mikosi/ balaa wanapoishi
Kazi zao zote zipate kuimarika vema
Wakapendwe na kusaidiwa na watu pale watakapokwama
Chonde, muwaone watoto na wajukuu wenu hawa
Babu, bibi na ndugu zetu wote mliolala hapa
Mtusikie kuomba kwetu (Tafsiri ).
**Chanzo:** Utafiti (2019)

Hapa tunaona kwamba, Wangoni kama jamii mojawapo ya Waafrika, wanaamini kuwa mizimu ina nguvu ya kuwaombea kwa Mungu ili waweze kuishi salama katika mazingira yao halisi. Imani hii hudokeza fikra za

kijaala zinazojikita katika kumtazama Mungu pekee kama mtatuzi na mfanikishaji wa mahitaji ya mwanadamu. Hii ni katika kuondokana na mabaya yote kama vile: mikosi kazini, kuchukiwa/kukataliwa bila sababu, na kupata maradhi yanayosumbua. Pia, mizimu huwasaidia walio hai kuweza kufanikiwa katika masuala mbalimbali ya kisiasa, kiuchumi, kielimu na kitaaluma. Suala hili hudhihirisha eskatolojia ya Waafrika ambapo huamini kuwa wafu bado wana thamani kubwa sana katika maisha ya walio hai. Mzimu ukichukizwa una nguvu ya kumfanya mkosaji kuishi katika hali ya tabu akiwa duniani. Katika kusisitiza zaidi jambo hili, mhojiwa mmoja anasema:

> Katika jamii yetu, mtu aliyekufa (*mahoka*) anatazamwa kwa namna ya heshima na thamani kubwa. Hii ni kwa sababu tunaamini kuwa, bado yupo pamoja nasi japokuwa hatumwoni kwa macho haya ya kawaida. Anatuona, anatusikia juu ya chochote tumwombacho na anatusaidia katika maisha yetu. Tunaamini kwamba, kule alikokwenda yupo jirani sana na Muumba wetu, hivyo ni rahisi kwake kutuombea sisi tuliopo duniani. Ukimkasirisha *mahoka* unaweza kupata balaa nyingi sana katika maisha yako. Kwa mafano, unaweza kulima eneo kubwa na usivune mazao mengi, familia inaweza kupatwa na maradhi mara kwa mara, kama umeajiriwa unaweza kusimamishwa kazi pasipo kosa lolote. Dawa ya hayo yote ni kufanya sadaka kwa ajili ya *mahoka* ili aweze/waweze kuridhika ndipo utafanikiwa. Kwetu sisi, ndugu wa damu aliyekufa hususani babu, bibi, baba na mama tunaamini kuwa wanatulinda na kutuwezesha au hutufanikishia masuala mbalimbali tuyatendayo. Hii ni kwa sababu wana uwezo wa kufanya maisha yetu yawe mazuri au mabaya kwa kuwa ana uwezo wa kukuombea kwa Mungu baba.

**Chanzo:** Utafiti (2019)

Katika nukuu hiyo tunaona kwamba Wangoni wanaamini katika mizimu kama suluhisho la mahitaji yao mbalimbali kwa kuwa ina nguvu ya kuwafanikishia mahitaji hayo. Hii ni falsafa ya Waafrika inayojidhihirisha kupitia eskatolojia ya jamii hiyo. Kwa hiyo, Wangoni kama jamii mojawapo inayoishi barani Afrika, wana eskatolojia inayodhihirisha Uafrika wao kupitia matendo mbalimbali.

## 5.0 Hitimisho

Kwa jumla, makala hii imejadili juu ya usawiri wa eskatolojia ya Waafrika katika mbolezi za Wangoni. Kabila la Wangoni hutumia mbolezi kama kijenzi muhimu katika kuomboleza kwenye matukio mbalimbali yanayoambatana na suala la kifo. Matukio hayo ni kama vile: katika ibada mbalimbali (wakati wa kuaga mwili wa marehemu nyumbani au kanisani na wakati wa kuzika makaburini) na matanga. Mbolezi hizo zimebainika kubeba masuala muhimu yanayodhihirisha kuwapo kwa eskatolojia ya Waafrika kulingana na tamaduni za kuamini kwao. Masuala hayo huhifadhi na kubeba maarifa mbalimbali yanayosawiri misingi ya maisha yao. Pia, mbolezi za Wangoni zimebainika kuhifadhi tamaduni za jamii hiyo zinazoendelezwa kwa namna ya kimapokeo kizazi hadi kizazi kingine. Hii ni kutokana na urithishwaji unaofanyika ambapo katika uimbaji huo, vijana wenye ari ya kuimba huhusishwa. Kwa kufanya hivyo, jamii hiyo inaendelea kudumisha suala la uimbaji katika matukio mbalimbali yanayoambatana na kifo kama suala muhimu katika kuomboleza kwao. Hivyo basi, katika makala hii masuala muhimu yaliyojadiliwa ni: kuamini katika uwepo wa Mungu, mwendelezo wa maisha baada ya kifo na kuamini katika nguvu za waliokufa (mizimu).

## Marejeleo


Baloyi, L. (2008). *The African Conception on Death: A Cultural Implication*. South Africa: University of South Africa.

Bujo, B. (1998). *The Ethical Dimension of Community: The African Model and the Dialogue between North and South*. Nairobi: Pauline Publications Africa.

Ebner, P. E. (2009). *The History of the Wangoni*. Ruvuma: Peramiho Printing Press.

Lup, J. R. (2013). Eschatology in a Secular Age: A Examination of the Use of Eschatology in the Philosophies of Heidegger, Berdyaer and Blumenberg. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). The University of South Florida. Inapatikana katika http/scholarcommons.usf.edu/cgi/viewcontent. cgi?article=5729/contex=etd.

Mapunda, G. C. (2016). *Humu za Kadeni na Chavatamii Vangoni: Hadithi za Zamani na Maisha ya Wangoni.* Dar es Salaam: *LOT Publication.*

Mbiti, J. S. (1990). *African religions and philosophies*. United Kingdom: Heineman Educational.

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: KAUTTU Limited.

Murphy, G. L. (2003). *African-American Faith in America*. New York: Oxford University Press.

Ngonyani, D. S. (1988). A Comparative Study of Kindendeule, Kingoni and Kimatengo. Tasnifu ya Umahiri (Hijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Oxford. (1989). *Oxford English Dictionary*. Nairobi: Oxford University Press.

Ponera, A. S. (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi*. Dar es Salaam: Karljamer print Technology.

Ponera, A. S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.

Ramose, M. B. (2002). *African philosophy thought of Ubuntu.* Harare, Zimbabwe: Mond Books Publishers.

Samuel, A. (1955). *Philosophy and Theology: Treasury of Philisophy*. New York: The Philosophical Library Inc.

Shields, J. M. (2008). *An Eschatological Imagination: A Revisionist Christian Eschatology in the Light of David Tracy's Theological Project*. New York: Peter Lang Publishing.

TUKI. (2014). *Kamusi ya Kiswhili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Open University Press.